

## **HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURACHA KAMATI YA FEDHA NA  
UTAWALA KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MAK TABA YA SHULE  
YA SEKONDARI MWENGE TAREHE 2/11/2021**

### **WALIOHUDHURIA**

- 1 Mh. Y.M.Kiaratu
- 2 Ndg. D. Luziga
- 3 Mh. H.S.Mkata
- 4 Mh. M.S.Ikaku
- 5 Mh. G.S.Mdama
- 6 Mh. I.S.Mrura
- 7 Mh. G.C.Mbuia
- 8 Mh. K.O.Munjori
- 9 Mh. H.H.Simba
- 10 Mh. R.E.Mande

### **WALIOHUDHURIA**

1. O.P.Simtengu
  2. A.R. Kamnde
  3. S. Mwaikenda
  4. A.Honorati
  5. T. John
  6. F.Kiyui
  7. B.Geban
  8. S. Manengo
  9. V. Odero
  10. Dr. A. Milulu
  11. Dr. A.Kalekezi
  12. T. Christopha
  13. B.Y.Mahenge
  14. T. Christopher
  15. F. Mshamu
  16. J. Gunda
  17. P. Msechu
  18. M.Mlingi
  19. G. Kazyoba
  23. J. M.Nzogu
  24. E. Venance
  - 25 J. Masuka
  26. M. Chale
  27. A.S. Mwendo
  28. V. Kavusha
- | <b>WAJUMBE</b>                 | <b>MWENYEKITI</b> |
|--------------------------------|-------------------|
| - Mstahiki Meya                | - KATIBU          |
| - Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa | -                 |
| - Naibu Meya                   | - Mjumbe          |
| - Diwani Kata ya Kisaki        | - Mjumbe          |
| - Diwani Kata ya Unyanga       | - Mjumbe          |
| - Diwani Kata ya Minga         | - Mjumbe          |
| - Diwani Kata ya Mtamaa        | - Mjumbe          |
| - Diwani Kata ya Utемини       | - Mjumbe          |
| - Diwani Viti Maalum           | - Mjumbe          |
| - Diwani Viti maalum           | - Mjumbe          |
- ### **WATENDAJI**
- |  |
|--|
| - Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala                   |
| - Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara                     |
| - Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari                 |
| - Mkuu wa Idara ya Mipangomiji na Ardhi                  |
| - Kaimu Mkuu wa Idara Mazingira na Udhibiti waTaka Ngumu |
| - Mkuu wa Idara ya Kilimo Umwagiliaji na Ushirika        |
| - Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani                   |
| - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango                         |
| - Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi                           |
| - Mganga Mkuu wa Manispaa                                |
| - Mkuu Idara ya Mifugo na Uvuvi                          |
| - Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii              |
| - Mkuu wa Kitengo cha Sheria                             |
| - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi                     |
| - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA                       |
| - Kaimu Mratibu wa miradi ya Benki ya Dunia              |
| - Afisa Habari   |
| - Meneja stendi ya Misuna                                |
| - Kaimu Mkuu kitengo cha Ufugaji Nyuki                   |
| - Mratibu wa TASAF                                       |
| - Afisa usafirishaji                                     |
| - Mwandishi wa Vikao                                     |
| - Mwandishi wa vikao                                     |
| - Afisa Tarafa Mungumaji                                 |
| - Afisa Tarafa Unyakumi                                  |

## **AGENDA**

1. Kufungua kikao
2. Taarifa ya Mapokezi ya fedha za UVIKO-19 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Shule
3. Kufunga kikao.

### **SMC/FA/MUHT.NA. 33/2021: KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe kwenye kikao cha dharura kilicholenga kupokea taarifa ya mgawanyo wa fedha za UVIKO-19 kwa ajili ya ujenzi wa Madarasa 42 ya Shule za Sekondari na Shule Shikizi. Mwenyekiti aliwataka Wajumbe kusikiliza kwa umakini taarifa hiyo kwa ajili ya usimamizi wa utekelezaji. Kikao kilifunguliwa saa 6.30 mchana.

### **SMC/FA/MUHT.NA. 34/2021: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UVIKO-19 ZA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA SHULE**

Taarifa iliwasilishwa ikionyesha kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Singida imepokea fedha kwa ajili ya kujenga Vyumba vya madarasa kwa Shule za Sekondari na Shule Shikizi. Taarifa iliwasilishwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Singida imepatiwa **Shs. 840,000,000** ambazo zimegawanyika katika maeneo mawili, **Shs. 680,000,000** kwa ajili ya Shule za Sekondari kwa vyumba 34 na **Shs. 160,000,000** kwa ajili ya Ujenzi wa madarasa 8 ya Shule Shikizi 4.

Pamoja na Mgawanyo huo, iliwasilishwa ombi la kubadilisha mradi katika Shule ya Sekondari Utetemi ambapo chumba kilichopangwa kujengwa katika Shule hiyo kihamishiwe katika Shule ya Sekondari Unyianga. Hii ni kutokana na hali ya ya ardhi katika Shule ya Utetemi kusababisha majengo katika Shule hiyo kupasuka, hivyo kupeleka ujenzi mwingine pale ni kuisababishia Serikali hasara. Eneo la Shule ya Sekondari Utetemi lina changamoto ambayo tayari imeshajadiliwa katika Vikao mbalimbali vya Halmashauri kiasi cha kufikia maamuzi ya kuangaliwa kwa eneo jingine kwa ajili ya kuihamisha Shule hii.

Wajumbe baada ya kupokea taarifa hiyo na kujadili walisema kuwa Kutokana na changamoto iliyopo shule ya Sekondari Utetemi, Wajumbe kwa kauli moja waliridhia Mpango huu wa maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19 upite pamoja na mabadiliko ya chumba cha darasa kihamishiwe katika Shule ya Sekondari Unyianga badala ya Utetemi

Aidha, Kamati kwa ujumla haikuridhika na mchakato uliopelekea kupatikana kwa fedha za Ujenzi wa Madarasa hayo yaliyopatiwa fedha katika upangaji wa fedha hizi. Kamati imeridhia utekelezaji wa miradi uendelee ili kutokwamisha malengo na muda wa utekelezaji wa miradi hii kama ilivyoelekezwa kutoka Serikali kuu.

Wajumbe waliazimia kuwa

## **AZIMIO**

Timu ya Menejimenti iwasilishwa mchakato mzima ulianzia wapi wa kupata mapungufu ya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa mwaka 2022 na vigezo vilivytumika kupata mapungufu hayo.

Baada ya maswali na ufanuzi mbalimbali Wajumbe wa Kikao kwa Kauli moja waliridhia Mpango huu wa UVIKO-19 wa ujenzi wa Miundombinu uendelee kama ifuatavyo:-

**MRADI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU KWA SHULE ZA SEKONDARI**

NA	SHUGHULI PANGWA	CHANZO CHA FEDHA	KIASI PANGWA
1	Kuwezesha Shule ya Sekondari ya Dk. Salmin kujenga darasa moja ifikapo Desemba, 2021	IMF	20,000,000.00
2	Kuwezesha Shule ya Sekondari Kimpungua kujenga darasa moja ifikapo Desemba, 2021	IMF	20,000,000.00
3	Kuwezesha Shule ya Sekondari Kindai kujenga vyumba 3 vya madarasa ifikapo Desemba, 2021	IMF	60,000,000.00
4	Kuiwezesha Shule ya Sekondari Mandewa kujenga vyumba 6 vya madarasa ifikapo Desemba, 2021	IMF	120,000,000.00
5	Kuiwezesha Shule ya Sekondari Mtamaa kujenga darasa moja ifikapo Desemba, 2021	IMF	20,000,000.00
6	Kuiwezesha Shule ya Sekondari Mtipa kujenga vyumba viwili vya madarasa ifikapo Desemba, 2021	IMF	40,000,000.00
7	Kuwezesha Shule ya Sekondari ya Mufumbu kujenga darasa moja ifikapo Desemba, 2021	IMF	20,000,000.00
8	Kuwezesha Shule ya Sekondari ya Mughanga kujenga vyumba 6 vya madarasa ifikapo Desemba, 2021	IMF	120,000,000.00
9	Kuiwezesha Shule ya Sekondari Mungumaji kujenga darasa moja ifikapo Desemba, 2021	IMF	20,000,000.00
10	Kuiwezesha Shule ya Sekondari Mwankoko kujenga vyumba viwili vya madarasa ifikapo Desemba, 2021	IMF	40,000,000.00
11	Kuiwezesha Shule ya Sekondari Senge kujenga vyumba 2 vya madarasa ifikapo Desemba, 2021	IMF	40,000,000.00
12	Kuiwezesha Shule ya Sekondari Unyambwa kujenga vyumba viwili vya madarasa ifikapo Desemba, 2021	IMF	40,000,000.00
13	Kuwezesha Shule ya Sekondari Unyamikumbi kujenga vyumba 2 vya madarasa ifikapo Desemba, 2021	IMF	40,000,000.00

<b>NA</b>	<b>SHUGHULI PANGWA</b>	<b>CHANZO CHA FEDHA</b>	<b>KIASI PANGWA</b>
14	Kuwezesha Shule ya Sekondari Unyianga kujenga darasa moja ifikapo Desemba, 2021	IMF	20,000,000.00
15	Kuwezesha Shule ya Sekondari Mitunduruni kujenga vyumba 3 vya madarasa ifikapo Desemba, 2021	IMF	60,000,000.00
<b>JUMLA</b>			<b>680,000,000.00</b>

#### **MRADI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU KWA SHULE ZA MSINGI**

<b>NA</b>	<b>SHUGHULI PANGWA</b>	<b>CHANZO CHA FEDHA</b>	<b>KIASI PANGWA</b>
1	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 2 katika Shule Shikizi ya Nkuhi ifikapo Desemba, 2021	IMF	40,000,000.00
2	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 2 katika Shule Shikizi Mwembemoja ifikapo Desemba, 2021	IMF	40,000,000.00
3	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 2 katika Shule Shikizi Mwachichi ifikapo Desemba, 2021	IMF	40,000,000.00
4	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 2 katika Shule Shikizi Sundu ifikapo Desemba, 2021	IMF	40,000,000.00
<b>JUMLA</b>			<b>160,000,000.00</b>
<b>JUMLA KUU</b>			<b>840,000,000.00</b>

#### **SMC/FA/MUHT.NA.35/2021: KUFUNGA KIKAO.**

Kabla ya kufunga kikao, Katibu aliwashukuru Wajumbe kwa michango yao iliyopelekea kuidhinishwa kwa Mpango huu. Alisema Mpango huu wa Ujenzi wa miundombinu ya Shule una ufuatiliaji katoka Taasisi zote za Serikali kuanzia Ngazi ya OR-TAMISEMI, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama. Katibu alisema Mradi huu unatakiwa kukamilika tarehe 15.12.2021 na kukabidhiwa. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itakuwa ikipatiwa Taarifa kila baada ya wiki mbili. Baada ya maelezo hayo alimkaribisha Mwenyekiti kufunga kikao. Naye Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa michango yao mizuri. Alisisitiza ufanuzi uwasilishwe kikao kijacho cha kamati ya Fedha na Utawala ili kuwa na utaratibu shirikishi wa upangaji wa miradi na kuwataka Waheshimiwa Madiwani wakatoe ushirikiano katika utekelezaji wa Miradi hii kwa maeneo yaliyopatiwa fedha za UVJKO-19. Mwenyekiti alifunga kikao majira ya Saa 7.30 mchana.

**"U M E T H I B I T I S H W A"**

SAINI ..... *Babuus* .....

SAINI ..... *Yuk* .....

JINA ..... *ZEFRIW* *IC* *Leibniz* .....

JINA ..... *YAGI M-KIBARATU* .....

**KATIBU**

*22/11/2021*

**TAREHE**

**MWENYEKITI**

*22/11/2021*

**TAREHE**